# Wanafunzi 200 kuonesha ugunduzi wa kisayansi

**Na Lucy Lyatuu**

WANAFUNZI takriban 200 kutoka shule mbalimbali za sekondari nchini, wanatarajia kuonesha kazi zao za teknolojia na ugunduzi wa kisayansi jambo litakaloendelea kuchochea ari na moyo wa wanafunzi kusoma kwa bidii masomo hayo ili kuleta manufaa kwa kizazi kijacho.

Kazi hizo za kisayansi zinatarajiwa kuoneshwa katika shindano linalotarajiwa kufanyika Agosti mosi hadi 2, mwaka huu. Wanafunzi nchini wamehimizwa kutuma kazi za miradi yao kwenda kwa Shirika la Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST) kabla ya Aprili 21, mwaka huu.

Kutokana na umuhimu wa maonesho hayo ambayo unalenga kuwainua wanafunzi kusoma masomo ya sayansi, Taasisi ya Karimjee Jivanjee (KJF) imeingia mkataba wa miaka mitano na YST kuanzia mwaka huu hadi 2022 ili kufadhili maonesho hayo kila mwaka kwa kutoa Sh milioni 226.

Akizungumza jana Dar es Salaam, Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk Gosbert Kamugisha alisema hadi sasa wameweza kupokea maombi 400 kutoka kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini.

Alisema wanasayansi chipukizi watakaoshiriki katika onesho la YST 2018 kwa sasa wanaendelea kutengeneza kazi za miradi yao katika nyanja mbalimbali za kisayansi kama kemia, fizikia na hesabu, baolojia na ekolojia, sayansi ya jamii na teknolojia.

"Kazi za miradi mingi zimejikita kutafuta suluhisho kuhusu matatizo katika sekta ya afya, kilimo na usalama wa chakula, mawasiliano, usafirishaji, nishati, elimu, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi," alisema Dk Kamugisha na kuongeza kuwa shule zote za binafsi na serikali nchini zinaruhusiwa kushiriki bila kutoa fedha yoyote.

Alisema wanafunzi watakaojituma na kufanya ugunduzi mzuri watazawadiwa fedha taslimu, medali, vikombe na uimarishaji wa maktaba ya shule zao.

Kama ambavyo imefanyika kwa miaka sita iliyopita, wanafunzi wenye ugunduzi mzuri zaidi watazawadiwa kupata udhamini wa masomo ya Chuo Kikuu ili kuwawezesha kusoma masomo ya sayansi na teknolojia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi kutoka KJF, Yusuf Karimjee alisema mfuko huo umejitoa kwa dhati kudhamini wanafunzi watakaoshinda katika shindano la kuonesha kazi za kisayansi kwa kuwa itasaidia kuinua nchi pamoja na kuhamasisha wanafunzi kusoma masomo hayo kwa kuwa sayansi ni muhimu katika maendeleo.